# Ufundishaji wa Fasihi ya Watoto katika Shule za Msingi Nchini Kenya

*Pamela M. Y. Ngugi*

*Ikisiri*

Fasihi ya watoto imeendelea kukua na kupanuka katika tanzu zake mbalimbali katika miaka ya hivi karibuni nchini Kenya. Fasihi hii imepata mwamko mpya tangu ijumuishwe katika muhtasari wa masomo ya lugha shuleni. Makala haya yanatathmini hali ya vitabu vya ziada kwa kuzingatia upatikanaji na ufaafu wake na kupendekeza namna watoto wa shule za msingi wanavyoweza kuelekezwa na kuhimizwa kusoma ili kujenga utamaduni wa usomaji miongoni mwao.

## 1.0 Utangulizi

Lengo mojawapo la ufundishaji wa Kiswahili kama somo nchini Kenya tangu mwaka 1981 ambapo Kiswahili kilijumuishwa katika muhtasari lilikuwa lingali ni kuhimiza na kuendeleza tabia ya usomaji miongoni mwa watoto, na vilevile kujenga ubunifu na kuendeleza mielekeo bora kuhusiana na matumizi ya Kiswahili kama lugha ya taifa na lugha rasmi (Taasisi ya Elimu, 2006). Fasihi ya watoto ilijumuishwa katika muhtasari wa somo la Kiswahili mwaka 2002 (Ministry of Education, 2002). Hatua hii ilichukuliwa baada ya wadau kutambua umuhimu wa fasihi katika kuendeleza lugha na kumkuza mtoto kijamii na kisaikolojia. Kutokana na uamuzi huu, kulihitajika tanzu mbalimbali za fasihi zifunzwe katika shule za msingi. Vilevile, uamuzi huu ulitokana na ugunduzi kuwa fasihi ya watoto ingeweza kutumika katika kutekeleza malengo ya jumla ya elimu. Lengo la makala haya ni kutathmini hali ya vitabu vya ziada hasa katika upande wa upatikanaji na ufaafu wake na kupendekeza namna watoto wa shule za msingi wanavyoweza kuelekezwa na kuhimizwa kusoma ili kujenga utamaduni wa usomaji miongoni mwao. Kabla ya kutathmini hali hii, hebu kwanza tueleze malengo mbalimbali ya kufundisha Kiswahili ili kufanikisha malengo ya kitaifa.

Malengo hutolewa kutokana na mahitaji ya kijamii. Kwa hiyo mafunzo yaliyoandaliwa kufanikilisha malengo hayo yalikusudiwa kutimiza mahitaji fulani ya kijamii. Katika muhtasari wa Kiswahili kwa ujumla, yapo malengo ya aina nne ambayo yote hutegemeana na kukamilishana. Malengo haya ni:

1. Malengo ya elimu ya kitaifa
2. Malengo ya elimu ya shule ya msingi
3. Malengo ya jumla ya kufundisha Kiswahili katika shule za msingi; na
4. Malengo maalumu.

Malengo haya yanahusiana na malengo maalumu kwa vile hutokana na malengo ya jumla ya kufundisha Kiswahili katika shule za msingi. Malengo ya jumla nayo yametokana na malengo ya elimu ya msingi. Nayo ya shule ya msingi yamekusudiwa kutimiza malengo ya elimu ya Kitaifa (Taasisi ya Elimu, 2006). Katika makala haya tutazingatia malengo ya kitaifa na malengo ya kufundisha Kiswahili ili tubainishe jinsi fasihi ya watoto inavyochangia katika kufanikisha malengo haya.

## 2.0 Malengo ya Elimu ya Kitaifa

Yapo malengo manane ya elimu ya taifa nchini Kenya. Malengo haya yameorodheshwa pamoja na maelezo mafupi ili kuonesha jinsi Kiswahili pamoja na fasihi ya watoto inavyochangia kuyatekeleza.

(i) *Kukuza utaifa, uzalendo na kuendeleza umoja wa kitaifa*

Kiswahili ni lugha ambayo hutumiwa kwa mawasiliano na idadi kubwa ya watu wa Kenya bila kujali makabila, dini, matabaka au rangi. Kwa hiyo, Kiswahili huchangia kuondoa nyufa zinazowatenga wanajamii. Kiswahili huchangia katika kudumisha umoja miongoni mwa wanajamii na huchangia kukuza utaifa, uzalendo na kuendeleza umoja wa taifa.

(ii) *Kuendeleza ujenzi wa taifa kiuchumi, kiteknolojia na kijamii*

Katika jamii yenye tamaduni nyingi, makabila mengi na lugha nyingi kama Kenya, ni muhimu kubaini lugha itakayotumiwa kwa ajili ya kuendeleza sayansi na teknolojia. Kiswahili kina mchango mkubwa wa kuwakabidhi wanafunzi mbinu bora za mawasiliano. Kupitia lugha hii, wanajamii wanaweza kufahamishwa kuhusu masuala ya kitaifa na yale yanayojiri katika safu za kimataifa.

(iii) *Kujiendeleza na kujiajiri binafsi*

Baada ya kupata masomo na kufuzu, Kiswahili kinamfungulia msomi fursa ya kujiendeleza na kujiajiri mwenyewe binafsi kwa kufanya kazi kama vile za sanaa au utunzi, utangazaji, uandishi na pia humpa mtu uwezo wa kuwasiliana katika kazi za biashara na nyinginezo.

(iv) *Kuendeleza uadilifu na amali za kidini*

Kiswahili hukuza mbinu zifaazo na mitazamo inayochangia uadilifu miongoni mwa wanafunzi ambao watakua wakiwa watu wenye

nidhamu, adabu na kujitegemea. Kupitia masomo mbalimbali, wanafunzi huelekezwa katika matumizi sahihi ya lugha.

(v) *Kuhimiza usawa wa kijamii na uwajibikaji*
Kiswahili hufunzwa katika viwango vyote na kutoa nafasi kwa Wakenya wote bila ubaguzi wa kijinsia, uwezo au mazingira.

(vi) *Kukuza, kuhifadhi na kuthamini tamaduni za jamii mbalimbali*
Wanafunzi wanahimizwa kukuza tamaduni muhimu katika ujenzi wa taifa. Kiswahili huweza kutekeleza jukumu hili kwa kuwafahamisha wanafunzi kuhusu wingi wa tamaduni katika jamii.

(vii) *Kuendeleza uhusiano wa kimataifa na kudumisha mwelekeo ufanao kwa mataifa mengine ulimwenguni*
Kiswahili ni lugha ambayo inafahamika katika nchi mbalimbali ulimwenguni kote. Lugha hii inaweza kutumika katika kurahisisha mawasiliano ulimwenguni, hasa miongoni mwa nchi zinazoitumia lugha hii. Halikadhalika, hufanya watu wa mataifa hayo wajihisi wamoja wanapowasiliana.

(viii) *Kuendeleza uhifadhi wa afya bora na mazingira*
Kiswahili hutumika hutoa mafunzo kuhusu afya na uhifadhi wa mazingira kupitia vitabu vya kiada na hata vya ziada (Taasisi ya Elimu Kenya, 2006).

Kwa sababu ya kutambua majukumu ya Kiswahili katika kutekeleza malengo haya, serikali ilijitolea kugharamia elimu ya msingi hasa kwa kutoa fedha za kununua vitabu vya ziada kwa shule zote za serikali nchini Kenya. Lengo lake lilikuwa kuhakikisha kuwa kila mtoto anaweza kupata vitabu viwili vya ziada.

Baada ya kurejelea malengo ya Elimu ya Taifa hebu sasa tuzingatie malengo yaliyowekwa ya kufundisha Kiswahili katika shule za msingi:

1. Kusikiliza na kuitikia vilivyo katika Kiswahili
2. Kuongea Kiswahili kwa ufasaha
3. Kusoma na kuelewa Kiswahili
4. Kujieleza kikamilifu kwa lugha ya Kiswahili kwa kuandika.
5. Kutunga kazi za kisanii kulingana na kiwango chake
6. Kuimarisha mazoea ya usomaji bora
7. Kupenda kujieleza katika somo la Kiswahili baada ya shule ya msingi
8. Kuonea fahari Kiswahili katika mawasiliano
9. Kutukuza na kuendeleza Kiswahili sanifu maishani

10. Kuthamini, kufurahia na kujivunia Kiswahili kama lugha ya taifa na ya kimataifa
11. Kutambua na kushiriki kupata suluhisho la masuala ibuka yanayohusu na kuathiri jamii kama vile afya na UKIMWI, uadilifu, jinsia, mazingira, haki na ajira za watoto (Taasisi ya Elimu Kenya, 2006).

Tunaona kuwa malengo haya yote yanaweza kufanikiwa kupitia ufundishaji wa fasihi ya watoto. Jambo la muhimu ni kutambua kuwa fasihi ya watoto inaweza kutumiwa katika kufundishia maeneo mbalimbali ya muhtasari.

## 3.0 Dhima ya Fasihi ya Watoto

Wataalamu wa fasihi ya watoto wamebainisha dhima kadhaa za fasihi ya watoto. Mojawapo ya dhima hizi ni kujiburudisha. Msomaji aliyebobea katika usomaji anaweza kutambua raha anayohisi katika kusafiri na mhusika fulani katika hadithi.

Dhima ya pili ya kusoma ni kutaka kujiondoa katika hali fulani ya matatizo anayopitia mtoto. Usomaji wa hadithi huwapa watoto nafasi ya kujisahaulisha au kuondoka kwa muda kwenye hali ya matatizo katika maisha. Dhima hii ni muhimu sio tu kwa watoto bali hata kwa watu wazima wanaohitaji kujiliwaza na kutoka kwa muda kwenye hali ngumu za kimaisha. Hata hivyo ni watu wachache wanaotambua namna usomaji wa vitabu unavyoweza kuwaliwaza.

Wasomaji-shabiki husoma kwa sababu wanafahamu kuwa vitabu huchachawisha ubunifu. Hadithi tunazozisoma hutufanya kufikiria kuhusu mhusika fulani, mazingira, sababu za kuwepo na mageuzi katika ploti, au kiishio cha hadithi ambacho ni tofauti na matarajio yetu.

Dhima nyingine ya fasihi ya watoto ni kwamba hutusaidia kujielewa na kuwaelewa watu wengine. Mtoto anakua akijua kuwa wapo watu ambao maisha yao ni tofauti na yake lakini ni muhimu kuwaheshimu na kukubali tofauti zao.

Mwisho ni kwamba watoto husoma ili waweze kupata uzoefu na kuelewa umbo la lugha. Watoto wanaweza kutambua matumizi mbalimbali ya lugha kupitia wahusika katika hadithi na baadaye kupata maarifa ya matumizi ya lugha ambayo yatamsaidia kujieleza vilivyo. Dhima hizi zinahusiana moja kwa moja na malengo ya elimu pamoja na malengo ya ufundishaji wa Kiswahili katika shule za msingi.

## 4.0 Upatikanaji, Ufaafu naUtendaji katika Fasihi ya Watoto

Katika sehemu hii tutaangazia mada hizi kwa kuonyesha jinsi fasihi ya watoto inavyokuzwa, kuendelezwa na kufunzwa kupita upatikanaji, ufaafu na utendaji.

### 4.1 Upatikanaji

Usomaji na ufundishaji wa fasihi ya watoto shuleni huathiriwa kwa kiasi kikubwa na hali mbalimbali, zikiwemo za upatikanaji wa vitabu. Tangu muhtasari mpya ulipoidhinishwa na kujumuisha fasihi ya watoto katika somo la Kiswahili, pamekuwapo na maendeleo makubwa katika upatikanaji wa vitabu vya ziada. Vitabu vya ziada ni vitabu vya nyongeza na huwa ni vitabu zaidi ya vile vya lazima katika kutimiza matakwa ya silabasi na hujumuisha vitabu vya picha, hadithi, tamthilia na ushairi ambavyo vimelenga viwango mbalimbali vya watoto kiumri na kijamii (Mbunda, 1983 na Muwanga, 2007). Kwa mujibu wa Kobia (2007), vitabu hivi husaidia kupanua stadi na maarifa yanayopatikana katika muhtasari.

Kwa ujumla, tunaweza kusema kuwa, kwa sasa vipo vitabu vingi vya ziada ambavyo vimechapishwa. Ukweli huu unaweza kudhihirika katika orodha ya vitabu vinavyopatikana katika *Approved List of Primary and Secondary Schools Textbooks and other Instructional Materials* maarufu kama "Orange Book". Kwa mfano, kufikia mwaka 2005 ni vitabu 101 tu vya Kiswahili vilivyokuwa vimeorodheshwa katika kitabu hiki. Kwa sasa tunavyo vitabu zaidi ya 400 (Ministry of Education, 2005 na 2011). Ingawa idadi ya vitabu imeongezeka, ni wazi kwamba ongezeko hilo ni la polepole mno likilinganishwa na vitabu vinavyopatikana vya Kiingereza. Vilevile, tangu mwaka 2003, serikali imechukua jukumu la kugharimia ununuzi wa vitabu vyote katika shule zote vikiwemo vya ziada, na hivyo kuhakikisha kwamba kila mtoto anapata nafasi ya kuvisoma vitabu hivi (Ngugi, 2010).

Baada ya walimu wakuu kupata orodha hii ya vitabu huwa ni jukumu la walimu wanaohusika kuviteua, kuagiza na kuvinunua vitabu hivi. Kwa ujumla uteuzi wa vitabu huongozwa na vigezo vifuatavyo:

- Mtindo sahili unaofaa katika utunzi wa vitabu vya watoto,
- Lugha inayoafiki kiwango cha utambuzi cha mtoto,
- Msamiati ulio wastani na usiwe mgumu sana wa kumlemea mtoto Wahusika ambao watoto wanaweza kujitambulisha nao na wawe wa kuaminika.

Hata hivyo, jambo muhimu la kizingatia katika uteuzi wa vitabu ni lile analopendekeza Green (1976) kwamba, iwapo tunataka kukuza na kuendeleza kipawa cha fasihi, na iwapo tunataka kutimiza shauku na matakwa ya watoto,

na pia iwapo tunataka kukuza na kujenga stadi za kusoma, basi vitabu vinavyopatikana maktabani sharti vichaguliwe kwa uangalifu. Hili linahitaji kuzingatiwa ili motisha ya usomaji wa watoto isiondolewe kabisa na vitabu visivyowavutia. Kwa hiyo, ni muhimu kuteua vitabu ambavyo vitasomwa na watoto wa viwango vyote bila kutegemea mtu mzima. Usomaji wa kujitegemea ndio unahitaji kuhimizwa ili kujenga mazoea ya kusoma.

Changamoto katika upatikanaji wa vitabu hivi kwa urahisi miongoni mwa watoto wa shule nyingi inatokana na sera za shule za uazimaji wa vitabu. Kwa mfano, utafiti uliofanywa na Ngugi (2010) ulionesha kwamba kuna changamoto nyingi kuhusiana na upatikanaji wa vitabu vya ziada shuleni. Baadhi ya walimu wakuu huegemea sana kununua vitabu vya kiada kuliko vitabu vya ziada. Bakka (2000) anaita hali hii, "Usomaji unaoegemea kwa vitabu vya Kiada." Hii inaweza kuwa na maana kwamba walimu wakuu wanachukulia kuwa ujifunzaji unaweza kuendelezwa tu kupitia vitabu vya kiada. Hawaoni umuhimu wa kujumuisha vitabu vya ziada. Ni vigumu kwa shule nyingi za mashambani kuvipata vitabu ambavyo vimeteuliwa kutoka kwenye "Orange Book" kutoka katika maduka ya uuzaji wa vitabu. Hii ina maana kuwa usambazwaji wa vitabu hauwafikii watoto walio katika maeneo ya mshambani.

Katika baadhi ya shule vitabu vinahifadhiwa katika ghala moja. Wakati mwingine vitabu huhifadhiwa kiholela tu, kwa mfano kuwekwa sakafuni.Ukosefu wa maktaba hasa katika shule za mashambani ambazo nyingi hazina majengo ya kudumu husababisha ubaribifu wa vitabu au hata huishia kuliwa na mchwa. Ukosefu wa maktaba unaweza kuchukuliwa kama ishara ya kutozingatia umuhimu wa usomaji wa ziada na wadau wa elimu (Krolak, 2005). Haya yote huwanyima watoto nafasi ya kukuza tabia ya usomaji. Ukosefu wa mkutubi anayeweza kuwaelekeza watoto maktabani ni tatizo kubwa katika shule nyingi. Utafiti umedhihirisha kwamba wakutubi huwa na nafasi kubwa katika kujenga mielekeo chanya ya usomaji miongoni mwa watoto na kuwafanya kuwa wasomaji mahiri (Usanga na Usoro, 2007). Shule nyingi hazina wakutubi na iwapo wapo, wengi huwa ni walimu ambao wamechaguliwa kusimamia maktaba ya shule. Kwa sababu hiyo, wengi hawana maarifa katika taaluma ya ukutubi na vilevile hawana nafasi ya kushughulikia watoto wakati wa kipindi cha maktaba kwa sababu huwa wana masomo mengine.

Mara nyingi watoto kunyimwa nafasi ya kuazima vitabu kwa sababu ya kuhofiwa kuvipoteza au kuviharibu. Iwapo mtoto atapoteza kitabu, mzazi anatakiwa kufidia, hivyo basi wazazi nao wanawakataza watoto wasiazime vitabu shuleni.

Aidha, darasa huwa limetengewa kipindi maalumu cha kuhudhuria makataba. Hata hivyo kutokana na baadhi ya sababu ambazo tumezitaja hapo awali, kipindi hiki mara nyingi hutumiwa kufunzia masomo mengine ambayo yanatahiniwa shuleni. Kutokana na kutozingatiwa kwa somo la maktaba pamoja na kupuuza umuhimu wa vitabu vya ziada, huwa hakuna kumbukumbu nzuri zinazowekwa kuhusu vitabu hivi. Kumbukumbu hizi zinaweza kuonesha tabia za usomaji kwa kila mtoto na hata katika shule nzima.

Katika shule nyingi, vitabu vya ziada huhifadhiwa katika ofisi ya mwalimu mkuu. Uwekaji wa vitabu katika ofisi ya mwalimu mkuu huwanyima watoto wasiokuwa jasiri nafasi ya kuazima vitabu hata kama watoto hawa wanafurahia kusoma vitabu vya ziada. Vitabu kama hivi vinahitaji kuwekwa mahali ambapo vitapatikana kwa urahisi kwa watoto wote mradi pawe na mpango maalumu wa kuviazima. Kila mtoto anapaswa kuwa na uhuru wa kuchagua vitabu kutokana na vitabu vingi vinavyopatikana katika maktaba iliyo karibu naye.

### 4.2 Ufaafu

Katika kipengele hiki, Wizara ya Elimu imetoa vigezo ambavyo vinahitaji kufuatwa na walimu wanaohusika katika uteuzi wa vitabu. Kwa ujumla ni kwamba vitabu vya ziada vimetolewa kulingana na viwango vya wanafunzi darasani. Hata hivyo, hiki si kigezo mwafaka cha kuwachagulia watoto vitabu tukizingatia kwamba kila mtoto ana shauku maalumu ya usomaji na vilevile kila mtoto ana uwezo tofauti wa kusoma. Hivyo, ufaafu wa uteuzi wa vitabu unahitaji kuongozwa na maswali yafutayo:

- Je, vitabu hivi vinafaa katika kiwango cha lugha cha wanafunzi wa darasa fulani?
- Mwanafuzi ataweza kuelewa maudhui yanayowasilishwa katika kitabu hicho?
- Je, mwalimu au mkutubi anafahamu hulka za wasomaji wake?

Changamoto zinazopatikana hapa ni kwamba walimu wengi si wasomaji wa vitabu vya watoto. Kwa hivyo, wengi wao hawawezi kuwateulia watoto vitabu kwa kuzingatia kigezo cha ufaafu. Kuna umuhimu wa kuwahimiza walimu kuwa wasomaji wa vitabu vya watoto ili wafahamu yaliyomo na waweze kufanya uteuzi unaofaa.

### 4.3 Utendaji

Utendaji ni zile kaida, au hali ambazo zinaongoza matumizi sahihi ya vitabu vya ziada shuleni. Kwa mfano, hurejelea ile namna ya kuwatanguliza watoto katika fasihi. Katika hali hii tunaangalia mikakati ya kuwapa watoto motisha ya kusoma. Katika utafiti uliofanywa na Ngugi (2009 na 2010) walimu

walioonekana kuwa na mielekeo chanya kuhusu vitabu vya ziada, baadhi wakidai kutumia mikakati ifuatayo kama njia ya kuwahimiza watoto: kuwapa watoto mazoezi ya kusoma, kuwa na majadiliano darasani kuhusu hadithi iliyosomwa, na kuwa na usomaji wa pamoja darasani.

Wataalamu kama vile Greenwood (1988) wanapinga mbinu ya kuwapa watoto mazoezi baada ya kusoma kitabu chochote cha fasihi kwa kudai kuwa mbinu hii hupunguza furaha na starehe ya kusoma. Katika hali kama hii tunaweza kuwahimiza watoto kwa kuwaeleza kuwa usomaji ni njia ya kujistarehesha na ili kupata starehe hiyo, ni muhimu kwa mwanafunzi kujibu maswali ili mwalimu ajue iwapo mwanafunzi ameielewa hadithi au la. Ni kutokana na sababu hii ndio maana baadhi ya wachapishaji hujumuisha maswali ya ufahamu katika vitabu vya hadithi.

Mijadala darasani ni muhimu kwa sababu huwapa watoto nafasi ya kutoa maoni yao kuhusu hadithi. Vilevile, hii inaweza kuwa mbinu ya kuwahimiza wanafunzi wasiopenda kusoma kujenga tabia za kusoma (Green, 1976) ili nao wajumuike katika mjadala.

Zipo mbinu kadha wa kadha ambazo zimependekezwa na wataalamu wa fasihi ya watoto na ambazo walimu wanaweza kuzishirikisha katika somo la fasihi na wanafunzi wao. Mbinu hizi zinaweza kutumika kabla ya usomaji kuanza, wakati wa usomaji na baada ya kumaliza kusoma kitabu. Mbinu zifuatazo zimependekezwa na Potyaeva (2005:345):

*Mbinu za Kuendeleza na Kuimarisha Usomaji*

| **Kabla ya Usomaji** | **Wakati wa Kusoma** | **Baada ya Kusoma** |
|---|---|---|
| • Utoaji wa maoni<br>• Ujengaji wa matarajio<br>• Ubashiri wa mwisho wa hadithi<br>• Uonyeshaji vielelezo<br>• Utoaji mifano<br>• Kufikiria kwa sauti<br>• Kuuliza maswali na kujadili<br>• Kuteua kitabu cha kusoma<br>• Usomaji wa kujitegemea | • Kusoma kwa sauti<br>• Kutunga nyimbo kutokana na hadithi<br>• Kuelekeza katika usomaji<br>• Kuwa na wakati wa kutulia na kufikiria<br>• Kusoma-kutulia—kujadili<br>• Kutalii kila sura ya hadithi<br>• Msomaji kujitathmini<br>• Kuwaza na kujenga taswira<br>• Kusikiliza na kusoma<br>• Usomaji kimakundi | • Mbinu za ufahamu<br>• Kutoa mahitimisho<br>• Kurejelea makala mengine na hata kuwa na ufahamu wa awali wa mambo<br>• Kujifunza mbinu za mpangilio wa makala<br>• Kukuza lugha |

Kwa ujumla, mambo yanayofanyika kabla ya kuanza kusoma hulenga kuwatia wanafunzi hamu na kukuza usomaji. Ni njia moja ya kuwapa motisha na vilevile huwasaidia wanafunzi kuielewa hadithi. Awamu hii inaweza kutoa mshawasha wa kusoma ili kumaliza kazi fulani au kuthibitisha hoja fulani. Kipindi cha "wakati wa usomaji" huzidisha ufahamu wa msomaji kumhimiza kuiangalia hadithi hiyo kwa makini zaidi kabla ya kumaliza kuisoma. Vilevile humsaidia mtoto msomaji kutafuta maana kutoka hadithini. Mbinu hii humsaidia mwalimu kukadiria uelewa wa wasomaji. Kipindi cha "Baada ya Usomaji" huhimiza kutafakari kuhusu yaliyomo hadithini, humsaidia msomaji kupanua na kukuza mitazamo yake kuhusu jambo fulani. Awamu hizi zote ni muhimu kwa sababu humpa mtoto nafasi ya kujieleza na kuingiliana na wenzake. Kama anavyodai Huck (1979), watoto hujifunza zaidi kuhusu vitabu ikiwa wanapewa nafasi ya kuvifasiri kwa njia ambayo inatoa maana kwao kupitia uchoraji au uigizaji, mijadala na uandishi.

Hata hivyo, katika shughuli hizi zote, huwa kuna changamoto nyingi zinazozuia utendaji zinazotokana na hali mbalimbali. Kwanza, walimu wengi kutowahusisha wanafunzi katika usomaji. Pili, walimu wenyewe si wasomaji wa vitabu vya watoto. Kwa hali hiyo, hawawezi kuongoza mjadala wa kusoma. Tatu, walimu wengi kukataa kujishughulisha na maswali ambayo hayatatahiniwa mwisho wa muhula au kwenye mtihani wa mwisho.

## 5.0 Jinsi ya Kukuza Utamaduni wa Kusoma miongoni mwa Watoto

Kutokana na kazi muhimu ambayo fasihi ya watoto hufanya katika kutekeleza majukumu ya elimu ya taifa pamoja na malengo ya kufunza Kiswahili mapendekezo yafuatayo yametolewa ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu haya kikamilifu. Kwanza, walimu wafundishwe mbinu za kujenga hamu miongoni mwa watoto kwa sababu tabia inayojengwa utotoni hudumu kwa muda mrefu. Pili, kuna umuhimu wa kupanua ubunifu na uelewa wa watoto kwa njia ya kusoma. Tatu, kuwapatia watoto mbinu mbalimbali za kusoma kulingana na mahitaji yao mbalimbali. Nne, kuwachochea na kuwashirikisha wazazi katika kuendeleza tabia ya kusoma ya watoto wao. Mwisho, kuwaelekeza watoto namna ya kutunza vitabu badala ya kuwanyima.

## 6.0 Hitimisho

Makala haya yameonesha jinsi fasihi ya watoto inavyoweza kutumika katika kufanikisha malengo ya elimu ya kitaifa na vilevile, kufanikisha malengo ya kufundishia Kiswahili. Tumeonesha hali ya fasihi ya watoto kwa kuzingatia mada tatu, upatikanaji, ufaafu na utendaji. Vilevile, tumeonesha changamoto zinatokea katika kujaribu kawaunganisha watoto na vitabu. Mwisho tumetoa mapendekezo ya jinsi ya kukuza mazoea ya kusoma miongoni mwa watoto.

## Marejeo


Bakka, P. (2000). "Back to books: Functional Literacy". Katika Kate Parry (mh.). *Langage and literacy in Uganda: Towards a Sustainable Reading Culture*. Kampala: Foundatain Publishers. Kur. 83-87.

Green, R. (1976). "Providing good Literature for young Children." Katika Lelan, B, Jakobs (wah). *Using Literature with Young Children*. New York: Teachers' College Press. Kur. 6-10.

Greenwood, J. (1988). *Class Readers*. New York: Oxford University Press.

Huck C. (1979). *Children's Literature in the Elementary School*. New York: Holt, Rinehart na Wington.

Kobia J.M. (2007). "Uandishi wa Vitabu vya Kiswahili katika Mfumo wa Elimu Nchini Kenya: Changamoto na Mapendekezo". Katika Kimani Njogu (Mh). *Kiswahili na Elimu Nchini Kenya*. Nairobi: Twaweza Communications. Kur. 28-42.

Krolak, L. (2005). The Role of Libraries in the creation of Literate Environment. UNESCO. Hamburg: Institute of Education.

Ministry of Education. (2005). *Approved List of Primary and Secondary Schools Textbooks and other Instructional Materials*. Nairobi: Ministry of Education.

Ministry of Education. (2010). *Approved List of Primary and Secondary Schools Textbooks and other Instructional Materials*. Nairobi: Ministry of Education.

Muwanga N. K. na wenzie. (2007). *Literacy Practices in Primary Schools in Uganda: Lessons for future Interventions*. Kampala: Fountain Publishers.

Ngugi, P. (2009). "Children's Literature in Kiswahili in Kenya: An Evaluation." Makala yaliyowasilishwa katika Institute of African Studies, Chuo Kikuu cha Vienna, Austria.

Ngugi, P. (2010). *Language and Literary Education: The State of Children's Literature in Kiswahili in Kenya*. Saarbrucken: Lambert Academic Publishing.

Potyaeva, T. (2005). "On the way to changing the future". Katika Gerry Shiel (mh) *Proceedings of the $14^{th}$ European Conference on Reading.* Zaghraeb, Croatia. Croatian Reading Association. Kur.345-347.

Rosenblatt, L. (1995). *Literature as Exploration*. New York: The Modern Language Assoation of America.

Stewig, J. W. (1980). *Children and Literature*. Chicago: Rand McNally College Publishing Company.

Taasisi ya Elimu, Kenya (2006). *Mwongozo wa Silabasi ya Kiswahili Kwa Shule za Msingi* 2002. Nairobi: Taasisi ya Elimu, Kenya.

Usanga, E. na Ima Usoro. (2007). "The Role of Nigerian Primary School Libraries in Literacy and Lifelong learning." http://www.encyclopedia.com.doc/IGI-162470505.html. 12.8.2011

*Makala haya yaliwasilishwa katika kongamano la CHAKITA lililofanyika Lenana Conference Centre, Nairobi, Agosti 2011 kuhusu Kiswahili na Ufundishaji.